**Deutsche Welle Radio**

**"Learning By Ear"**

**Jobs & Training 02: Makanika wa magari**

***Mwandishi: Pierre Kazoni***

***Wahariri: Ulrich Neumann, Maja Dreyer***

***Tafsiri-Kiswahili:Eric Ponda***

---

**1 Msimulizi.**

**4 Sauti: - Estelle, Makanika msichana**

**- Mamadi Ouedraogo, mmiliki Gareji**

**- Ali, Mekanika Mvulana**

**- Mamake Ouedraogo**

---

**Intro**

Hujambo na karibu kwa mfululizo wa vipindi vyetu vya Learning By Ear kuhusu kazi na Mafunzo, ambapo leo tunaangazia watu wenye taaluma mbali mbali. Pengine umesikia kuhusu kazi zinazochukuliwa kuwa za wanaume pekee. Kwa Mfano kazi ya Makanika au kurekebisha magari. Imebainika kwamba Barani Africa, kunahitaji kubwa la wafanyi kazi katika sekta hii. Katika miji mikubwa, utakuta magari mengi barabarani ilihali sehemu za mashambani ni Beiskeli na Pikipiki zinazotumiwa sana.

Lakini ni wanawake wachache tu unaoweza kumbana nao wakishughulika kurekebisha magari katika Gareji nyingi za mijini. Hivi leo kutana na Estelle Christian Ouedraogo kutoka nchini Bukina Faso anayeishi mjini Ouagadougou. Jiji lenye idadi kubwa ya Beiskeli na Pikipiki na hata kubandikwa jina la Mji wa Beskeli na Pikipiki. Estelle mwenye umri wa miaka 20 hufanaya kazi katika mji huu kama makanika.

**1. O-Ton Estelle (Frz)**

Najaribu kurekebisha hii kabureta ambayo inasababisha gari hili lisiwake. Imejaa uchafu ndani! Hii jeti yake ni chafu na nikifaulu kutoa huu uchafu ndani basi gari litawaka mara moja bila matatizo.

**2. SFX Mngurumo wa Gari**

**3. O-Ton Estelle (Frz)**

Hii kazi ya kurekebisha magari naipenda sana. Sijawahi kuona makanika mwanamke na ndio sababu niliamua kujitosa katika sekta hii. Muajiri wangu anaitwa Mamadi Ouedraogo.

**3. SFX Sauti za barabarani na Gareji.**

Mamadi ni mmliki wa Gareji anakofanya kazi Estelle. Gareji hiyo hupatikana kando kando mwa barabara moja yenye shughuli nyingi na inauwezo wa kurekebisha magari 30 kwa siku. Licha ya Shughuli nyingi Gareji hii inadumisha usafi na vifaa vyote vya kudumisha usafi vinapatikana hapa.Utakuta kwamba Estelle anatumia jina la familia ya Bosi wake, lakini kwamwe hawana uhusiano wowote. Je Mamadi anamchukuliaje Estelle kama Makanika mwanamke.

**5. O-Ton Mamadi Ouedraogo (Frz)**

Kwanza napenda kazi yake sana. Yeye ni mjasiri na navutiwa na ujasiri huo. Amewapa changamoto vijana wengi wa eneo hili, na ni ajabu sana kuona mwanamke aliyejitolea kwa dhati kama Estelle, kufanya kazi ya makanika wa kurekebisha pikipiki na baiskeli. Hii ni changamoto kubwa kwa wasichana wengine!

Kuna uhusiano mzuri baina ya Estelle na bosi wake, na kila mmoja katika gereji hiyo hufurahia kufanya kazi na Estelle, kama asemavyo mfanyakazi mwenzake Ali.

**6. O-Ton Ali (Frz)**

Mimi hufurahia kazi ya Estelle, kwani ana ujuzi wa hali ya juu. Daima huhakikisha kazi aliyoifanya kwa kufanyia majaribio, yaani *testi* barabarani pikipiki au baiskeli aliyoirekebisha yeye mwenyewe, kabla ya kumkabidhi mwenyewe..

**7. SFX Makelele ya Gareji.**

Estelle, wafanyi kazi wenzake na hata Bosi wake pia wamevalia ma- ovaroli ya rangi ya Samawati, yaliyojaa Grisi kila mahali hata mikononi. Gareji hiyo ina jumla ya wafanyi kazi sita wa kiume pamoja na Estelle. Estelle anasema kuwa hadhalilishwi na wenzake wa kiume kwani wote wanaujuzi sawa na wanalipwa na muajiri huyo mmoja.

**8. O-Ton Estelle (Frz)**

Hapa hakuna mvutano, tunaheshimiana kama watu wanaofanya kazi pamoja. Sisi tunamfanyia kazi bosi wetu kwa moyo mmoja bila ya kubaguana. Kwa hiyo mchango wangu unawaridhisha wafanyakazi wenzangu na hata wateja.

**7. SFX Makelele ya Gareji.**

Baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu, Estelle anamini amepata ujuzi wa kutosha anaohitaji kuanzisha gareji yake na kuisimamia yeye mwenyewe.

**9. O-Ton Estelle (Frz)**

Nafikiria kuanzisha gereji yangu binafsi katika muda wa miezi miwili ijayo. Na ikiwa nitakuwa na pesa za kutosha pia nitafungua duka la vipuri na kuwaajiri vijana hasa wasichana ambao wako tayari kufanya kazi ya makanika kama mimi!

**7. SFXMakelele ya Gareji.**

Mjini Ouagadougou na pia miji mingi nchini Bukina Faso, wengi wa vijana hawana ajira na wamesalia kuhangaika huku na kule wakitafuta ajira. Estelle anafahamu tatizo hili la ukosefu wa ajira na kila mara huwashauri vijana wenzake kutatufa kazi yoyote kufanya ili kujipatia angalau riziki kidogo.

**10. O-Ton Estelle (Frz)**

Mimi huwambia vijana wenzangu kazi ya Makanika ni nzuri na inamapato. Wale walioko barabarani wakitafuta ajira wanapasa kujiunga nami tufanye kazi pamoja. Kila mara huwashauri wasikae ovyo kurandaranda ua kuomba omba, kwani huenda wakashawishika kuingiza katika matendo maovu kama vile wizi. Wanapasa kujiepusha kabisa na maovu hayo.

Estelle alipata mafunzo yake ya umakanika katika chuo kinachotoa mafunzo hayo mjini Koudougou, umbali wa kilomita 100 magharibi mwa mwa Mji wa Ouagadougou.

**11. O-Ton Estelle (Frz)**

Taasisi hiyo inatoa mafunzo ya umakani kabisa kwa wasichana pekee. Tulikuwa wasichana tisa na sote tulipita mtihani na kukabidhiwa vyeti vya kufuzu. Lakini sio waalimu wote waliokuwa makanika chuoni humo kwani tulikuwa tukisomea masomo manne. Kwa mfano masomo ya nadharia, utendaji, uhasibu na elimu ya utawala wa umma, yalikuwa yakifunzwa na mkufunzi kutoka idara ya masuala ya kijamii.

Ingawa Estelle hajaolewa na kujaliiwa kuwa na familia, anafahamu fika majukumu anayopasa kutekeleza kama mwanamke nyumbani. Baada ya kazi hurudi nyumbani kuwasaidia wazazi wake na kazi za nyumbani.

**12.O-Ton Estelle (Frz)**

Mimi humsaidia mama yangu na kazi za nyumbani, kisha baada ya kutayarisha chakula cha jioni na kula pamoja, hupiga gumzo kabla ya kulala. Kila mara wazazi wangu hunishauri mimi na dada zangu wadogo. Baba pia hunishauri kuhusu umuhimu wa kumheshimu bosi wangu, wafanyakazi wenzangu na wateja kwa jumla. Hata mteja akikugombeza pasi na sababu unapasa kumnyenyekea kwani ni yeye ndiye unayemtumikia.

Wakati wa mazungumzo mezani, Mamake Estelle hugusia masaibu wanayokumbana nayo wasichana wanaotafuta ajira.

**13. O-Ton Mama Estelle(Frz)**

Wizi au kufanya ukahaba si vizuri. Mimi humshauri msichana wangu Estelle kuzingatia kazi yake kwani maisha si rahisi. Wanawake wengi hupenda kutegemea mabwana wanaofanya kazi. Mungu awasaidie wasichana wengine wawe kama binti yangu.

Wazazi wake wanajivunia Estele kwa kazi yake. Lakini je wanaume wanawachukuliaje wanawake wanaofanya kazi chafu chafu ya kujipaka grisi kila mahali?
Estelle anachekeshwa na swali hilo.....

**14. O-Ton Estelle (Frz)**

(***Akicheka****)* Swali hilo linanifurahisha lakini nitalijibu tu. Urembo si hoja kwa wanaume wenye akili zao. Wanachotafuta kwa mwanamke ni tabia na msichana anayeweza kujitegemea. Mimi nina wavulana wanaonitongoza licha ya harufu ya grisi na mafuta ya petroli.

**15. SFX Sauti za Watu / Gareji**

**Outro**

Basi Mumemsikia Estelle kutoka gareji yake iliyoko mjini Ouagadougou, nchini Burkina Faso Yeye aliamua kujifunza kazi ya Makanika, kurekebisha magari na Piki Piki na sasa anafanya kazi kama Makanika mwanamke. Licha ya kazi hii kuonekana yenye kumletea pato zuri, bado inadharauliwa na wasichana wengi Barani Africa. Basi kufikia hapo hatuna budi kutia nanga kipindi cha leo cha Learning By Ear, Noa bongo jenga maisha yako, kilicho angazia taaluma. Pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri.